# UFUGAJI BORA WA KUKU WA ASILI



# UTANGULIZI

- Zaidi ya Watanzania 86% ni wakulima na wafugaji.

- Wafugaji wa kuku wa asili wanakadiliwa kufikia milioni 56 ambao wanachangia 30% ya pato la jumla litokanalo na mifugo

# 1.SIFA,CHANGAMOTO NA FAIDA ZA UFUGAJI KUKU WA ASILI

SIFA

- kustaimili magonjwa
- Nyama nzuri.
- Uwezo mzuri wa **kutotoa**,**kulea vifaranga**.
- Uwezo mzuri wa **kujitafutia chakula**

# CHANGAMOTO

- Hutoa mazao machache sana (mayai&nyama).(mayai **50-90** badala ya **100-150**)

- Uzito wa kuku hai ni wa chini sana **1.0-1.5 kg** badala ya **1.8-2.5 kg**

# FAIDA ZA UFUGAJI WA KUKU WA ASILI

# MAYAI & NYAMA





# MBOLEA






# MAGANDA YA MAYAI
# (CHAKULA CHA MIFUGO)





# KUONGEZA KIPATO





# CHAKULA CHA SAMAKI



# MAPUNGUFU YA UFUGAJI WA KUKU WA ASILI

- Magonjwa
- Mabanda duni
- Tabia na miiko ya baadhi ya jamii.
- Wezi,wanyama na ndege
- hupatikanaji haba wa chanjo

# 2.KABILA MBALIMBALI ZA KUKU WA ASILI

KUCHI

- Uzito jogoo 3.5kg,mitetea 2kg
- Uzito wa mayai - 45g

Maeneo - Mwanza,shinyanga,tabora na Zanzibar

# KUCHI



# UMBO LA KATI

- Uzito wa majogoo **1.9kg**, mitetea **1.1kg**
- Mayai - **43g**
- Hukua haraka & uwezo mkubwa wa kujikinga na ugonjwa wa **NCD**.
- Hupatikana karibia maeneo yote ya Tanzania.

# KUKU WA UMBO LA KATI



# INAENDELEA……

- (iii) Ching’wekwe
- (iv) Singamagazi
- (v) Mbeya
- (vi) Pemba
- (vii) Unguja
- (viii)Kishingo
- (ix)Nungunungu

# 3.MIFUMO YA UFUGAJI WA KUKU

- (i) Ufugaji huria
- (ii) Ufugaji nusu huria
- (iii) Ufugaji wa ndani

# (i) UFUGAJI HURIA

- Ufugaji wa asili

FAIDA

- Hauna gharama

CHANGAMOTO

- Magonjwa,uzalishaji duni,wezi, & upatikanaji duni wa kumbukumbu
- Tumia hekari 1 kwa kuku 100

# UFUGAJI HURIA





# (ii) UFUGAJI NUSU HURIA

- Kuku hupewa chakula cha ziada&banda bora lenye uzio.

FAIDA ZA UFUGAJI HUU

- Uzalishaji bora,ulinzi,utunzanji wa kumbukumbu

CHANGAMOTO

- Ni wa gharama ukilinganisha na mfumo wa huria





# (iii) UFUGAJI WA NDANI

- Katika mfumo huu kuku ufungiwa ndani ya banda muda wote.

FAIDA ZA MFUMO HUU

- Uzalishaji mkubwa,udhibiti wa **magonjwa**,wezi & utunzaji bora wa kumbukumbu.

CHANGAMOTO

- Gharama

# UFUGAJI WA NDANI



# 4.MAANDALIZI YA UFUGAJI WA KUKU WA ASILI

**Banda bora**

- Panafikika kwa urahisi.
- Pasituamishe maji.
- Pasiwe pa mwelekeo wa upepo mkali

# BANDA BORA



# SIFA ZA BANDA BORA LA KUKU

- paa imara
- Kuta zisiwe na nyufa
- Hewa ya kutosha .
- uwezo wa kuingia mtu wa kufanya usafi
- Liwe na  nafasi inayolingana na idadi ya wastani wa kuku.
- Mfano;kuku 10-15/$m^2$  (HURIA)

NUSU HURIA kuku 4 - 8 ili kuruhusu nafasi ya vyombo vya **chakula** na **maji**.

# KUCHAGUA KUKU WA KUENDELEZA KIZAZI

- Chagua kuku kulinganisha na uzalishaji wa wazazi

SIFA

- Kutaga mayai mengi,umbo kubwa na uzito mkubwa
- Boresha kwa kutumia majogoo ya kisasa

# SIFA ZA KUZINGATIA WAKATI WA KUCHAGUA MITETEA

- Umbile kubwa.
- Uwezo wa kutaga wakiwa na umri mdogo (miezi 6).
- Uwezo wa kustahimili magonjwa.
- Uwezo wa kukua haraka.
- Uwezo wa kutaga mayai mengi {zaidi ya 15 kwa mtago mmoja (clutch).
- Uwezo wa kuatamia na kuangua vifaranga wengi na kuwalea.



# SIFA ZA KUZINGATIA WAKATI WA KUCHAGUA MAJOGOO

- Umbo kubwa
- Miguu imara na yenye nguvu
- Kucha fupi
- Mwenye nguvu
- Machachari
- Upanga/kilemba kikubwa
- Uwezo wa kuitia chakula mitetea
- Tabia ya kupenda vifaranga

# MAJOGOO BORA





# FAIDA YA KUONDOA KUKU WASIOFAA KWENYE KUNDI

- kuongeza uzalishaji(mayai)
- Inapunguza gharama ya chakula
- Inapunguza uenezaji wa magonjwa
- Huongeza nafasi zaidi kwa kuku
- Uwezekano wa kuuza kuku kama hao ni mkubwa kabla hawajafa

# UMRI WA KUPEVUKA

- Mitetea huanza kutaga wakiwa na umri wa miezi 6 - 8
- Jogoo huanza kupanda akiwa na umri wa miezi 7 lakini mbegu zake huwa bado kukomaa.
- Hutoa mbegu zilizokomaa anapofikia umri wa miezi 10
- Uwiano wa mitetea na majogoo 1-10:12

# FUGA KUKU UPATE FAIDA KWA KUZINGATIA


- Uthibiti wa magonjwa
- Weka kumbukumbu (mapato & matumizi)
- Gawa mapato yatokanayo na ufugaji wa kuku kwa matumizi yako (33%), maendeleo ya mradi (34%), na akiba (33%)

# 5.VIFAA MUHIMU NDANI YA BANDA LA KUKU

- Vyombo vya Chakula
- Vyombo vya Maji
- Viota
- Vichanja, na
- Matandiko

# VYOMBO VYA CHAKULA NA MAJI

- Vyombo vya chakula usaidia kuzuia upotevu wa chakula
- Vyombo vya maji ni vyema vikaning'inizwa kuzuia maji kuchafuliwa na kumwagwa kwa huraisi.


5"



# VIOTA



# VICHANJA VYA KUPUMZIKIA NA MATANDIKO

- Sifa za kichanja(urefu mita 1 toka ardhini,vijiti vya juu vyapaswa kuwa vya duara).

- Aina za matandiko(mabaki ya  mpunga na landa za mbao)- upana wa matandiko 5-10cm


9:26 AM Sat Nov 9 2013 39°F
HenCam

# 6.VYAKULA NA ULISHAJI WA KUKU WA ASILI

- Ili kuku watoe mazao bora wanaitaji chakula kilicho gawanyika katika makundi 5.

- Protini (mashudu,dagaa & wadudu)
- Wanga (pumba,ulezi & mtama)
- Vitamini (mboga za majani)
- Madini (mifupa & chokaa ya mifugo)
- Maji

# INAENDELEA....

- Mfano wa kiasi cha chakula cha ziada kwa kulisha kwa siku kuku wa kienyeji 5 na vifaranga 15

- Jogoo mmoja - 1 x 65 gm = 65 gm
- Mitetea - 4 x 65 gm = 260 gm
- Vifaranga - 15 x 25 gm = 375 gm
- **Jumla 700 g**

# MCHANGANYIKO WA CHAKULA CHA

| AINA YA CHAKULA | VIFARANGA | WANAOKUA | WAZAZI | WENGINEO |
|---|---|---|---|---|
| Mahindi yaliyo barazwa | 8 | 8 | 8 | 10 |
| Pumba za mahindi | 20 | 20 | 20 | 25 |
| Mashudu ya Alizeti | 8 | 7 | 10 | 6 |
| Unga wa dagaaa | 6 | 6 | 3.5 | 3 |
| Unga wa mifupa | 0.75 | 1.5 | 3 | 1 |
| Chokaa ya mifugo | 1.75 | 2 | 4 | 4 |
| Chumvi ya mezani | 0.5 | 0.5 | 0.5 | 0.5 |
| Soya iliyobalazwa | 3 | 3 | - | - |
| Unga wa damu | 1 | 1 | - | - |
| premix | 1 | 1 | - | 0.5 |
| Egg Booster | - | - | - | - |
| JUMLA | **50** | **50** | **50** | **50** |

# 7. UTAGAJI, UATAMIAJI NA UANGUAJI WA VIFARANGA

- Kuku wa kienyeji uanza kutaga wakiwa na miezi 6-8
- Viota viandaliwe wakiwa na umri wa miezi 4-5

# FUATA UTARATIBU UFUATAO KUHIFADHI MAYAI

- Sehemu ya yai iliyochongoka iwe chini na pana iwe juu.
- Hifadhi sehemu yenye kupitisha hewa ya kutosha na isiyokuwa na joto (25-27 $^{o}$c)
- Mayai yasikae kwenye hifadhi hiyo zaidi ya (2wk) toka siku yalipotagwa.



# SIFA ZA MAYAI YA KUATAMIWA

- Masafi
- Yasiwe na nyufa
- Yatokane na kuku aliyepandwa na jogoo
- Ukubwa wa wastani
- Yasiwe ya mviringo (mpira) au ncha kali
- Yasikae zaidi ya 2 wk
- Yasiwe yaliyohifadhiwa kwenye sehemu yenye joto( > 27 $^{o}$c)

# AINA ZA MAYAI





# NJIA ZA UATAMIAJI NA UANGUAJI

Kuna njia mbili za uatamiaji na uanguaji.

- Kubuni
- Asili

# UATAMIAJI NA UANGUAJI WA KUBUNI

- Njia hii uhusisha utumiaji wa mashine(incubator)
- Faida za njia hii

✓ mayai mengi kuatamiwa kwa wakati mmoja

✓ Kupata vifaranga wengi kwa wakati mmoja

✓ Ni njia bora zaidi kwa wafanya bihashara wa kuku



# CHANGAMOTO ZA UTUMIAJI WA MASHINE ZA KUTOTOLESHEA VIFARANGA

- Utaalam
- Muda
- Ni wa gharama-incubator
- Nishati ya huakika
- Uangalizi

# UATAMIAJI NA UANGUAJI WA ASILI

- Kwa kawaida kuku anatakiwa kuatamia mayai (12-15) kwa wakati mmoja kufuatana na umbile la kuku.

FAIDA ZA UAGUAJI WA ASILI

- Gharama nafuu
- Hakuna haja ya wafanyakazi
- Ni njia nyepesi kwa maeneo ya vijijini
- Hakuna maitaji ya elimu kwa mfugaji



# CHANGAMOTO ZA UAGUAJI WA ASILI

- Uzalishai duni( mtetea 1 mayai 12-15)
- Ufanisi wa uaguaji utegemea mazingira husika(baridi & joto)
- Upunguza uzalishaji wa kuku kwa mwaka ( mayai 90-150)

# KUWATAYARISHA KUKU WA KUATAMIA

- Hakikisha kwamba hawana chawa, utitiri au viroboto.

**Vitu vya kufanya ili kuuwa wadudu**.

- Toa matandiko *(litter)* ndani ya kiota.
- Nyunyiza dawa ya kuua wadudu
- Pia mnyunyizie dawa kuku anayetarajiwa kuatamia.



# KUWAFANYA KUKU WENGI KUTOTOA KWA WAKATI MMOJA

Fanya yafuatayo

- weka alama kila yai linalotagwa (namba au tarehe)
- Yanapofika mayai 3 yaondoe (weka mayai bandia)
- Anapoanza kuatamia unaweza kumuongezea mayai bandia (8 -10)
- Fanya hivyo kwa kila kuku (pata idadi sahihi ya mayai)
- Chagua mayai ya kuatamia ukianza na yai la mwisho kutagwa (wawekee mayai usiku)


# MBINU ZA KUZALISHA KUKU WENGI KWA MUDA MFUPI


- Mafanikio ya mpango huu hupatikana kwa kuwanyang'anya kuku vifaranga vyao pale vinapotototolewa (siku 1), na baada ya **siku 14** kuku hurudia tena kutaga.
- Kwa kutumia njia hii kuku mmoja anaweza taga mpaka mayai 248/mwaka.



# JINSI YA KUTAMBUA MAYAI YASIO NA MBEGU

- hatua hii ufanya siku ya 7-10 tangu mayai yaanze kuatamiwa
- Tumia mwanga mkali kumulika yai ndani ya chumba chenye giza
- Yai lenye mbegu uonyesha mishipa ya damu na lisilo na mbegu huwa cheupe kabisa


Egg
Candling
Embryo
Development
Summary
light provided by
The IncuBright™
Egg Candler
Copyright
Incubator Warehouse 2014
Day 3
Day 6
Day 8
Day 10
Day 15
Day 19



# 8.ULEAJI WA VIFARANGA

- Uleaji wa vifaranga ni hatua ya mwanzo ya ufugaji wa kuku
- Vifaranga uitaji joto kwa muda wa(1-4 wk) za mwanzo
- Kwa kutumia mitetea vifaranga hupata joto kwa muda wa siku 90

# MIFUMO YA ULEAJI WA VIFARANGA

- (i) mfumo wa asili
- (ii) mfumo wa kubuni

# MFUMO WA ASILI

- Vifaranga ulelewa na mtetea kwa muda wa siku 90

**Faida za mfumo huu**

- Ni wa gharama nafuu
- Vifaranga hupata mafunzo kutoka kwa mtetea
- Usaidia kuku wasiugue magonjwa kama Marek's.

# CHANGAMOTO ZA MFUMO WA ASILI

- Vifaranga kufa kwa baridi kama mtetea si mzuri kwa uleaji
- Hatari ya wanyama na ndege kwa viranga
- Sio mfumo mzuri kibiashara



# MFUMO WA KUBUNI

- Mfumo huu hautumii mtetea wakati wa uleaji wa vifaranga
- Utumika zaidi kwa wafugaji wanaofuga kibiashara
- Vifaranga huwekwa kwenye kifaa cha joto(bruda) kwa muda usiozidi wiki 4

# FAIDA ZA MFUMO HUU

- Ni mfumo mzuri kibihashara
- Vifaranga huwa katika uangalizi salama
- huzuia vifo vya vifaranga

# CHANGAMOTO ZA MFUMO WA KUBUNI

- Ni wa gharama (nishati ya umeme)
- Muda (Uangalizi wa vifaranga)
- Magonjwa kuenea ka kasi kama kuku wengi wakirundikana eneo moja.








# UTUMIAJI WA BRUDA

- Bruda ni moja kati ya nyenzo muhimu kwa uleaji wa vifaranga kwa njia ya kubuni
- Vifaranga ukaa ndani ya bruda kwa muda husio zidi wiki 1-4
- Uwiano wa vifaranga ndani ya bruda ni 16 vifaranga/1m square

# MWONEKANO WA VIFARANGA NDANI YA BRUDA

(i) joto liko sawa


Mara nyingi vifaranga huwa wachangamfu huku wakila chakula na kukimbia kimbia ndani ya bruda


Chombo cha
chakula
Vifaranga
Chombo
cha maji

# INAENDELEA.....

(ii) joto limezidi


Vifaranga wataonekana kua mbali na chanzo cha joto huku wakiwa  wametanua mabawa na kunywa maji kwa wingi



# INAENDELEA.....

(iii) joto alitoshi


- kuku ujikusanya kuzunguka chanzo cha joto/wenyewe kwa wenyewe
- Kukosa hamu ya kula



# INAENDELEA……

(iv) Upepo mkali

- Vifaranga kukimbilia sehemu moja ya banda ni kiashiria cha huwepo wa upepo mkali
- Upepo mkali uathiri vifaranga kutokana na baridi


Upepo

# 9.TABIA MBAYA ZINAZOWEZA KUJITOKEZA MIONGONI MWA KUKU WA ASILI

(i) Ulaji wa mayai

(ii) kudonoana

# (i) ULAJI WA MAYAI

Sababu

- tabia ya kurithi
- Chakula chenye upungu wa protini na madini kama calcium (Ca)
- Msongamano ( viota vichache ndani ya banda)
- Kuku kuwa na sehemu moja tu ya kulala na kutaga



# (ii) KUDONOANA

Sababu

- Msongamano mkubwa wa kuku ndani ya banda  ( viota vichache ndani ya banda)
- Chakula chenye upungu wa Protini na madini kama Calcium (Ca)





# 10. MAGONJWA NA WADUDU WASHAMBULIAO KUKU WA ASILI

Baadhi ya magonjwa yashambuliao kuku wa asili

- Kideri/Mdondo *(New Castle Disease)*
- Ndui ya kuku *(Fowl pox)*
- Kipindupindu cha Kuku *(Fowl Cholera)*
- Mafua ya kuku *(Infectious Coryza)*
- Homa ya matumbo *(Fowl Typhoid)*
- Kuhara damu *(Coccidiosis)*
- Ukosefu wa Vitamini A
- Minyoo na wadudu kama viroboto, chawa, utitiri na kupe wa kuku

# (i) KIDERI/MDONDO *(NEW CASTLE DISEASE)*

- Ugonjwa huu uwapata kuku wakubwa na wadogo-90%-100% ya kuku hufa.
- Ugonjwa huu husababishwa na virusi na huweza kushambulia pia bata, bata mzinga, kanga, kwale na ndege wengineo.

**Jinsi unavyoambukiza**

- Hewa
- Kuku mgonjwa
- Mizoga ya kuku
- Kinyesi cha kuku
- Vyombo vya usafiri

# DALILI ZAKE

- Homa kali,  kuwa dhaifu, kuzubaa na kushusha mabawa na kupoteza hamu ya kula.
- kupoteza fahamu na kupooza viungo.
- Kulegea kwa shingo na inaweza kupinda kuelekea nyuma au pembeni pia huweza kuzungusha shingo.
- Kuhema kwa shida na hutoa majimaji mdomoni yenye harufu kali

# INAENDELEA….

- Kukohoa, kukoroma na kupiga chafya.
- Kuharisha kinyesi chenye rangi ya kijani.
- Vifo vya mfululizo vinavyoweza kumaliza kuku wote bandani

# INAENDELEA.....






# MATIBABU YA KIDERI

- Ugonjwa huu unaambukizwa na virusi, hivyo basi hauna tiba, bali kinga tu
- **Muhimu:** Usichanje kuku kama ugonjwa umeshaingia kwenye kundi

# INAENDELEA….

- Chanjo za kideri/mdondo zimegawanyika katika makundi 2.

(i) Inayoweza kuvumilia joto (thermastable)

Chanjo hii inaweza kutunzwa katika joto la kawaida kwa muda wa siku 7

(ii) Isiyovumila joto

- Huifadhiwa kwenye friji muda wote
- Kuku hupewa ndani ya maji kwa muda wa masaa 2 tu.

# KUKU WAKIPEWA CHANJO YA KIDERI



# KIDERI V

# 2.NDUI YA KUKU *(FOWL POX)*

- Ugonjwa huu usababishwa na virusi
- Huathiri kuku wadogo zaidi ukilinganisha na kuku wakubwa.

MATIBABU

- Ugonjwa huu hauna tiba
- Kuku wapewe chanjo ndani ya 6wk.

# JINSI UGONJWA UNAVYOAMBUKIZWA

- Kupitia kwenye vijeraha vya kuku
- Usambazwa na Mbu

DALILI ZAKE

- Homa kali,kupoteza hamu ya kula&kupoteza uzito
- Kutokea kwa vipele sehemu zisizokuwa na manyoya(baada ya siku 7-14 vipele upasuka na kutoa vidonda)
- Kutoa makamasi kwenye pua
- vifo



# NDUI V

# 3.HOMA YA MATUMBO *(FOWL TYPHOID)*

- Ugonjwa huu husababishwa na bacteria
- Ushambulia kuku wakubwa na wadogo

Njia ya maambukizo

- Mayai
- Kuku wenye ugonjwa (kinyesi cha kuku)
- Watu na vyombo vya usafiri
- Mizoga ya kuku

# INAENDELEA…

## Dalili

- Homa kali.
- Manyoya husimama.
- Kinyesi kuonekana kuganda sehemu ya nyuma.
- Kukosa hamu ya kula.
- Kuku kudhoofika.
- Kiwango cha utagaji hushuka.

# INAENDELA…

## Kinga

- Tenganisha vifaranga na kuku wakubwa.
- Kuku wagonjwa watengwe na kupewa tiba ya *antibiotic.*
- Zingatia usafi wa banda na vyombo vya chakula na maji

## Matibabu

- Dawa aina ya *Oxytetracycline (OTC) au Salfa ambayo huchanganywa kwenye maji na kupewa* kuku kwa siku 5 hadi 7

# 4.MAFUA YA KUKU *(INFECTIOUS CORYZA)*

- Ugonjwa huu usababishwa na bacteria wapatikanao sehemu zenye mavumbi
- Ushambulia hasa kuku wakubwa

Jinsi unavyoambukiza

- Kuku asiye mgonjwa kula chakula au kuvuta hewa yenye vimelea vya ugonjwa huu.
- Kuku wazima wanapochanganywa na wagonjwa

# INAENDELEA…..

## Dalili

- Kuvimba uso chini na nyuma ya jicho
- Kupumua kwa matatizo na hata kukoroma
- Kuvimba kwa macho
- Kushindwa kula
- Kutoka makamasi puani
- Kutoa usaha unaonuka

# INAENDELEA....

Kinga

- Tenganisha vifaranga na kuku wakubwa.
- Kuku wagonjwa watengwe na kupewa tiba ya *antibiotic.*
- usafi wa banda na vyombo vya chakula na maji

Matibabu: Dawa za Salfa au *Antibiotic*

# KUKU WENYE MAFUA





# MAFUA V

# 5.KUHARA DAMU *(COCCIDIOSIS)*

- Ugonjwa huu usababishwa na vimelea aina ya *protozoa*
- Ushambulia kuku wakubwa na wadogo (huathiri zaidi kuku wadogo)

## Jinsi unavyoambukiza

- Kula chakula chenye kinyesi au maji yenye vimelea vya ugonjwa huu

# INAENDELEA.....

Dalili

- Kuharisha kinyesi kilichochanganyika na damu
- Kuku kudhoofu na kupungua uzito
- Kuku kuzubaa na kushusha mabawa (kavaa koti)
- Kuku kujitenga na wengine
- Kupoteza hamu ya kula

Tiba

- Dawa aina ya *Amprolium, Oxytetracycline au Salfa* (siku 5-7)

# INAENDELEA……

Kinga

- Vifaranga wakifikia umri wa siku 7 wapewe Amprolium kwa siku tatu 3 mfululizo
- Tenganisha vifaranga na kuku wakubwa
- Kuku wagonjwa watengwe na kupewa tiba mara moja
- Usafi wa banda,vyombo vya chakula&maji

# KUKU WENYE UGONJWA WA COCCIDIOSIS







# COCCI V

# 6.KIPINDUPINDU CHA KUKU *(FOWL CHOLERA)*

- Kipindupindu cha kuku husababishwa na bakteria

Dalili

- Kuharisha kinyesi cha njano
- Kusinzia na kulegea
- Kuhema kwa shida
- Kushindwa kusimama
- Kulala huku kichwa kimening’inizwa kwenye mabawa
- Kuwa na uvimbe kwenye mikunjo ya miguu

# KIPINDUPINDU CHA KUKU





# INAENDELEA….

## Tiba

- Dawa aina ya *Oxytetracycline (OTC) au Salfa* ambayo huchanganywa kwenye maji siku(5-7)

## Kinga

- Chanja kuku wakiwa na umri wa miezi (3).
- Usafi wa banda na vyombo vya chakula na maji

# 7.UPUNGUFU WA VITAMIN “A”

- Utokea kwa kuku kutokana na upunngufu wa madini ya vitamia A( hasa kipindi cha kiangazi)

Dalili za ukosefu wa vitamini ‘A’

- Kuku kudumaa kutokana na kutokula vizuri.
- Macho huvimba na kutoa uchafu mzito kama sabuni iliyolowana

Tiba

- Hakuna tiba itakayomponyesha kuku baada ya dalili hizi kujitokeza na matokeo yake ni kifo.
- Kuku wapatiwe *multivitamin*

# INAENDELEA……..

Kinga

- Hakikisha kuku wanapata majani ya kijani katika malisho yao
- Wapatie kuku *Multivitamin* kipindi cha kiangazi



# 8.WADUDU WASHAMBULIAO KUKU WA ASILI

- Kuku ushambuliwa na wadudu mbalimbali ambao wamegawanyika katika makundi (2)

(i) wanaoshambulia ndani ya mwili

(ii) wanaoshambulia nje ya mwili(juu ya ngozi)

# (i) WANAOSHAMBULIA NDANI YA MWILI

## Minyoo

- Kuna minyoo ya aina nyingi inayoshambulia kuku na kusababisha kupungua kwa utagaji na udhoofu wa kuku.
- Minyoo ya mviringo *(Ascaris)* hushambulia sana kuku na kusababisha madhara makubwa

# INAENDELEA…..

Dalili za minyoo

- Upungufu wa hamu ya kula
- Kudumaa kwa kuku wanaokua
- Kupungua kwa utagaji
- Minyoo mingine husababisha kupumua kwa shida
- Kuku hupungua uzito
- Minyoo kuonekana kwenye kinyesi



# INAENDELEA…….

Kutibu na kuzuia minyoo

- Minyoo mingi huuliwa na dawa ya *Piperazine*
- Wapatie kuku dawa ya minyoo kila baada ya miezi 3
- Usafi wa mabanda na kuzuia unyevunyevu

# (ii) WANAOSHAMBULIA NJE YA MWILI (JUU YA NGOZI)

- Hawa ni wadudu wanakaa kwenye manyoya na ngozi (chawa,utitili,papasi & viroboto)

**Viroboto, Chawa, Utitiri, Kupe, Papasi**

- Viroboto ni tatizo kubwa kwa vifaranga, hunyonya damu hadi kuua.
- Utitiri hunyonya damu na huathiri sana kuku wanaoatamia.

# INAENDELEA…..

Chanzo cha kuwepo wadudu

- Mipasuko sakafuni na kwenye kuta
- Uchafu uliokithiri
- Kuingiza kuku wageni

Dalili

- Kufubaa kwa manyoya
- Rangi ya upanga kuwa hafifu kutokana na upungufu wa damu
- Kukosa hamu ya chakula
- Ngozi kuwa nene, ngumu na yenye magamba yanayodondoka kama unga mweupe
- Kupungua uzito
- Kujikunakuna kwa kuku
- Wadudu kuonekana kwa macho

# INAENDELEA….

Athari za wadudu washambuliao kuku

- Kuku anayeatamia hatulii kwenye kiota
- Kupungua au kukoma kwa utagaji
- Ukuaji wa taratibu
- Ulaji hafifu



# RATIBA YA CHANJO YA KUKU

| SIKU | CHANJO | NJIA YA UTOAJI CHANJO |
|---|---|---|
| Ya 1 | kupooza(mareks) | sindano(subcutaneous) |
| Ya 7 | Mdondo/kideri | Maji/Matone |
| Ya 14 | Gumboro(IBD) | Maji |
| Ya 28 | Mdondo/kideri ,rudia kila baada ya miezi 3 | Maji/Matone |
| Wiki ya 6 | Ndui ya kuku(Fowl Pox) | Sindano kwenye mbawa |
| Wiki ya 12 | Dawa ya minyoo | Levatec/Levamid |
| Wiki ya 17 | Wape OTC plus ili kuimalisha kinga ya mfumo wa mwili | maji |

# MUHIMU

- Magonjwa ni chanzo kikuu cha vifo kwa kuku wa Asili na hii husababisha hasara katika ufugaji, Kinga ni bora kuliko tiba
- Fanya usafi wa mabanda
- Usafi wa vyombo vya chakula & maji
- Pata ushauri kutoka kwa wataalam
- Kuku wageni watengwe kwa muda usiopungua siku 14 kabla hawajachanganywa na kuku wenyeji

# 11: TIBA ZA ASILI

- Madawa ya asili yatokanayo na mimea yana weza kutumia kama tiba ya magonjwa mbalimbali ya kuku.
- Sehumu za mmea zitumikazo ni:Majani,mizizi,magome na matawi

**UMUHIMU WA TIBA ASILI**

- Hupatikana kwa urahisi.
- Ni rahisi kutumia.
- Gharama nafuu.
- Zinatibu vizuri.
- Hazina madhara

# (i) MWAROBAINI

- Majani, Mizizi & Magome



**HUTIBU**

- Typhoid.
- Kuzuia Kideri.
- Kuhara.
- Mafua.
- Vidonda

# (ii) SHUBIRI MWITU *(Aloe vera)*

- Chukua majani 3-5, katakata na loweka ndani ya maji lita 10-12/saa.
- Wape  kwa siku 5-7/tengeneza nyingine baada ya masaa 12



**HUTIBU**

- Kideri
- Homa ya matumbo *(Typhoid)*
- Mafua *(Coryza)*
- Kipindupindu cha kuku

# (iii) MTAKALANG’ONYO *(Euphorbia)*

- Majani makubwa 3-5, ponda/10L za maji kwa masaa 12-16, chuja na wape kuku

**HUTIBU**

- Kideri
- Gumboro
- Ndui
- Kuhara damu *(Coccidiosis)*



# (iv) NDULELE *(Dungurusi, Makonde, Tura/Ndula)*

- Majani hutibu Minyoo.
- Matunda hutibu Vidonda



# (v) PAPAI *(Majani)*

- Chemsha majani 2/maji lita 6 hadi ubakie na lita 1, Poza kisha chuja.

**Hutibu**

- Minyoo



# (vi) MINYAA *(Cactus)*

- Angalia inaunguza au kubabua.

**HUTIBU**

- Vidonda.
- Ngozi.
- Uzazi.



# (vii) PILIPILI KICHAA

- Pondaponda kiasi kisha changanya na maji.
- Inasaidia kutibu KIDERI (lakini mapema kabla maradhi kuingia)



**MIFUGO PLUS GROUP**
**CALL/WHATSAPP 0747 608 608**
**0762 212 142**
**TEGETA||GOBA**

**TUNAUZA VIFAA AINA VYOTE VYA UFUGAJI WA KUKU KAMA VILE;**

**Cages za kisasa za kuku wa mayai na nyama.|kuku wa kubwa na vifaranga|**
**Mashine za kisasa za kutotoleshea vifaranga|full automatic incubator|kuanzia mayai 16 hadi 15000.**
**Taa za joto maalumu za kulelea vifaranga|Infrared| 4 heater za feni za kulelea vifaranga.**

**5 vifaa vyote vya kuundia**

**mashine|incubator**

**accessories| 6 Nipple za**

**kunyweshea maji Kuku.**

**7 Mzani wa digital wa kupima**

**chakula cha kuku|kg**

**50|kg300| 8 Tunafunga**

**mifumo yote ya kunyweshea**

**maji kuku na chakula.**

9. **Tunajenga mabanda ya kisasa ya ufugaji kuku.**

12. **Tunauza mashine ya yakutengeneza chakula chenga chenga cha kuku|manual|automatic|**
13. **Tunauza hydroponics fodder tray.**
14. **Tunauza tochi maalumu ya kupimia yai lenye mbegu.**
15. **Tunauza digatal hygrometer|kipima**

**joto bandani na incubator| 16**

**Tunauza grinder and mixer machine.**

**17 Tunauza mashine ya kukatia kuku midomo|manual|automatic|**